

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA



Ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango Fedha na Utawala)

MAWASILIANO YA NDANI

KWA: Watumishi wote

KUTOKA: Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Fedha na Utawala)

TAREHE: 05.07.2023

**YAH: UJAZAJI WA MALENGO YA UTENDAJI KAZI KWA MWAKA 2023/2024
(OPRA ANNUAL TARGET 2023/2024)**

Itakumbukwa kwamba Kanuni za Utumishi wa Umma (2022) zinamtaka kila mtumishi wa umma kuandaa malengo ya utendaji kazi kila ifikapo mwanzoni wa mwaka mpya wa fedha kwa kushirikiana na kiongozi wake, Malengo ya utendaji kazi yanapaswa kuendana na mpango Mkakati wa Taasisi (**Rolling Strategic Plan**). Kwa msingi huo nawakumbusha watumishi wote pamoja na viongozi wao kutekeleza takwa hilo la kikanuni kwa kujaza malengo ya kazi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yanayoendana na mpango mkakati wa chuo (OUT Rolling Strategic Plan)

Wakuu wa vitivo/kurugenzi/vituo vya mikoa na Vitengo mnakumbushwa kushirikiana na watumishi walio chini ya mamlaka zenu kukamilisha zoezi hili kwa wakati. Utaratibu wa jinsi ya kuwasilisha malengo hayo utatangazwa baadae.

Wakati huo huo tunawakumbusha pia uwasilishaji wa **“Annual Review 2022/2023” umefungwa** na kama kuna mtumishi ambaye hajawasilisha fomu yake awasiliane na kiongozi wake.

Nawashukuru kwa ushirikiano wenu,

Francis Badundwa

K.N.Y: Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Fedha na Utawala)